TANZANIA COFFEE BOARD

bbt Building a Better Tomorrow




# Mradi Wa Kuongeza Unywaji Wa Kahawa Nchini kupitia Migahawa Inayotembea

AJENDA 10/30
KILIMO NI BIASHARA

# UTANGULIZI

**Sekta** ya kahawa Tanzania katika mkakati wa miaka mitano umeweka lengo la kuongeza soko la ndani kwa kahawa kutoka asilimia 7 ya sasa mpaka 15 ya uzalishaji wa kahawa nchini. Ili kuweza kufikia lengo hili Wizara ya Kilimo kupitia Bodi ya Kahawa imebuni aina mpya ya migahawa inayotembea (Mobile coffee shop) kwa lengo la kuwafikia wanywaji wa kahawa mahali walipo na hivyo kuwajengea utamaduni wa kunywa kahawa.

## 2. MRADI WA MIGAHAWA YA KAHAWA INATEMBEA

Migahawa hii itasimamiwa kupitia mradi wa BBT – kuongeza ushiriki wa vijana kwenye mnyonyoro wa thamani wa kahawa. Ambapo vijana watakaoshiriki watapewa mikopo ya kuendesha migahawa hii na pindi watakapo maliza kulipa mikopo hiyo watamilikishwa.

Fedha zitakazokusanywa kutokana na marejesho ya waliokopeshwa zitatumika kutengenezea migahawa mingine ya kuendelea kukupeshwa kwa vijana wengine.

## 3. UTEKELEZAJI WA MRADI

Ili kutekeleza mradi huu Bodi ya Kahawa imeshirikiana na taasis za fedha kutengeneza bidhaa ya mkopo ambayo itatolewa kwa vijana kwa riba na masharti nafuu. Vijana watakaoshiriki mbali na kupewa elimu ya usimamizi wa fedha pia watapewa mafunzo ya utayarishaji wa kinywaji cha kahawa kwa kutumia mashine za kisasa (Barista training).

## 4. BIDHAA YA MKOPO WA MIGAHAWA INAYOTEMBEA.

Bidhaa hii ya mkopo wa migahawa inayotembea itakuwa na vitu vifuatavyo;

I. Pikipiki ya miguu mitatu (Bajaji) iliyotengenezwa maalum kwa ajili ya kutumika kama mgahawa.
II. Mashine ya kutengeneza kahawa (expresso machine)
III. Mashine ya kusagia kahawa (grinder)
IV. Boksi la kutunza ubaridi (cooler box) kwa ajili ya kutunza maziwa.
V. Mfumo wa Umeme kwa ajili ya kuendeshea mashine ya kutengeneza kahawa




KAHAWA HOUSE
TANCAFE
Kwa maisha yenye Furaha
info@coffee.go.tz
Simu:+255 27 2752324
TANCAFE
Kwa maisha yenye Furaha
info@coffee.go.tz
Simu:+255 27 2752324
MC383 EDK